## HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI
## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA
## TAREHE 02 NOVEMBA, 2021 KATIKA OFISI YA AFISA MIPANGO

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:-**

1. Ramlah Munisi - MWENYEKITI
2. Dennis L. Mmbando - KATIBU
3. Mariam H. Hassan - MJUMBE
4. Fadhili Chimsala - MJUMBE
5. Edina A. Palla - MJUMBE
6. Dr. Furaha Mwakafwila - MJUMBE
7. Cosmas Nsemwa - MSHAURI

**WAKARIBISHWA**

1. Joseph Komanya - Mweka hazina

**SEKRETARIETI**

Charles P. Mpenzu - Afisa Ugavi.

**AGENDA:**

1. Kufungua kikao.
2. Kusoma na Kuthibitisha agenda za tarehe 02/11/2021.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 18/10/2021.
4. Yatokanayo na kikao cha tarehe 18/10/2021
5. Kujadili na Kupitisha manunuzi yaliyofanyika kwa njia ya Circular Resolution.
6. Kujadili na Kupitisha Ununuzi wa Matairi ya Magari Idara ya Afya
7. Kujadili na Kupitisha Njia ya manunuzi utekelezaji wa Fedha za Mradi wa Maendeleo kwa kutumia fedha ya uviko 19
8. Kujadili na kupitisha Wazabuni/Maduka ya Kutoa huduma ya vifaa vya Ujenzi kwa kutumia mfumo wa "Force Accounts"
9. Kujadili na kupitisha manunuzi yatakayo fanyika kwa ujumla (Bulk Procurement) Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo Uviko 19 kwa shule za msingi na sekondari.
10. Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti
11. Kufunga kikao.

**MUHT. NA. 21/2021/2022 – KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 08:30 Mchana kwa kuwakaribisha wajumbe waliohudhuria na kuwaambia kuwa ni kikao cha Bodi cha kawaida. Baada ya kufungua kikao Mwenyekiti aliwaomba wajumbe kuwa makini ili kutoa maamuzi sahihi yatakayokuwa na manufaa kwa Halmashauri yetu.

**MUHT. NA. 22/2021/2022 – KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA ZA TAREHE 02/11/2021**

Wajumbe walizipitia Agenda za kikao na wakakubaliana kuwa zipo sahihi kuwa zijadiliwe.

**MUHT. NA. 23/2021/2022 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 18/10/2021.**

Wajumbe walisoma muhtasari ukurasa kwa ukurasa na Kufanya masahihisho , baada ya kusoma walikubaliana kuwa haya ndiyo yaliyojadiliwa kikao kilichopita, muhtasari upo sahihi na usainiwe kuwa kumbukumbu halali za ofisi.

**MUHT.NA 24/2021/2022 - YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 18/10/2021.**

Hakukuwa na yatokanayo kwa kikao kilichopita

**MUHT.NA.25/2021/2022- KUPITISHA MANUNUZI YALIYOFANYIKA KWA NJIA YA CIRCULAR RESOLUTION.**

Katibu aliwasilisha manunuzi yaliyofanyika kwa njia ya Circular Resolution kwa wajumbe wa Bodi ya zabuni ambayo yalikuwa ni kama ifuatavyo-:

- Manunuzi yaliyofanyika kwa Circular Resolution ni kama ifuatavyo-:

| NA. | JINA LA MZABUNI | MAELEZO | KIASI | TAREHE | IDARA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | NASSOR SERVICE STATION | Diesel | 16,000,000 | 22.10.2021 | ELIMU MSINGI |
| 2 | NASSOR SERVICE STATION | Diesel | 3,465,000 | 23.10.2021 | AFYA |
| 3 | NASSOR SERVICE STATION | Diesel | 3,712,000 | 26.10.2021 | ELIMU SEKONDARI |

Wajumbe waliridhia kuwa manunuzi haya ndio waliyoyapitisha kwa njia ya maandishi "Circular Resolution" .

**MUHT.NA. 26/2021/2022: KUJADILI NA KUPITISHA UNUNUZI WA MATAIRI YA MAGARI IDARA YA AFYA**

Katibu aliwasilisha manunuzi ya Matairi ya magari ya idara ya Afya (Hospitali ya Wilaya) Yaliyofanyika kwa njia ya mfumo wa kielectroniki (TANePS)

Ununuzi wa Matairi ya Magari wazabuni walioomba ni kama ifuatavyo:-

| Na. | JINA LA MZABUNI | KIASI |
|---|---|---|
| 01. | JUBILEE TYRES P.O.BOX 1032 ARUSHA | 8,333,920.00 |
| 02. | AZZA HAMISI MOHAMED P.O.BOX 626 SINGIDA | 10,630,000.00 |

Wajumbe baada ya kupitia na kujadili walimpitisha **Jubilee Tyres P.O.Box 1032 Arusha** Kufanya kazi ya kuuza Matairi ya Magari gharama ya Tsh. **8,333,920.00.**

**MUHT.NA. 27/2021/2022: KUJADILI NA KUPITISHA NJIA YA MANUNUZI UTEKELEZAJI WA FEDHA ZA MRADI WA MAENDELEO KWA KUTUMIA FEDHA YA UVIKO 19**

Kujadili na Kupitisha Njia ya manunuzi utekelezaji wa Fedha za Maendeleo kwa Kutumia Fedha za Uvico 19 katika Shule za Msingi, Sekondari na Hospitali ya Wilaya

Mchanganuo wa mgao wa fedha hizo ni kama ifuatavyo-:

| Na. | KITUO | KIASI | CHANZO CHA FEDHA | AINA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shule za Msingi | 1,840,000,000 | MPANGO WA MAENDELEO UVICO 19 (TCRP) | Ujenzi wa Madarasa |
| 2 | Shule za Sekondari | 960,000,000 | MPANGO WA MAENDELEO UVICO 19 (TCRP) | Ujenzi wa Madarasa |
| 3 | Hospitali ya Wilaya | 300,000,000 | MPANGO WA MAENDELEO UVICO 19 (TCRP) | Ujenzi wa Madarasa |
| 4 | Ujnenzi Kituo Cha Afya Chibumagwa | 250,000,000 | SERIKALI KUU | Umaliziaji kituo cha Afya Chibumagwa |
| 5 | Shule ya Msingi Sayuni | 80,000,000 | MPANGO WA MAENDELEO UVICO 19 (TCRP) | Ujenzi wa Bweni |
| 6 | Shule ya Sekondari Manyoni | 31,872,379.85 | P4R | Uchimbaji wa kisima na Ujenzi wa Miundombinu ya Maji |
| 7 | Shule ya Msingi Kitalalo | 31,872,379.85 | P4R | Uchimbaji wa kisima na Ujenzi wa Miundombinu ya Maji |
| 8 | Shule ya Msingi Londoni | 11,972,379.85 | P4R | Uchimbaji wa kisima na Ujenzi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | wa Miundombinu ya Maji |
| | **JUMLA KUU** | **3,505,717,139.55** | | |

Wajumbe waliipokea na kujadili na kuazimia kuwa utekelezaji wa mradi huu utekelezwe kwa njia ya "Force Account" na Pia pale inapowezekana watumike pia wakandarasi bila kuadhiri bajeti iliyopangwa.

**MUHT.NA. 28/2021/2022: KUJADILI NA KUPITISHA WAZABUNI/MADUKA YA KUTOA HUDUMA YA VIFAA VYA UJENZI KWA KUTUMIA MFUMO WA "FORCE ACCOUNTS"**

Katibu aliwasilisha Orodha ya Maduka ya kuuza vifaa vya ujenzi kwa taasisi za serikali na hili linatokana na Muongozo mpya wa Manunuzi kutoka wakala wa manunuzi na Ugavi (PPRA) wa mwezi meyi 2020 unaotaka taasisi ambazo hazina maduka au wazabuji karibu ya kuuza vifaa vya ujenzi yaliyoidhinishwa na GPSA kwa ajili ya miradi inayotekelezwa kwa njia ya Force Account Kuoredhesha maduka yaliyopo na Kuidhinishwa na Bodi ya Manunuzi na Hapa na nukuu "**According to Guideline for Carrying Works under Force Account Reg. 32, 32.2 The list of suppliers/shops shall be identified from the community surrounding the entity , where there are no suppliers shortlisted by Government Procurement Service Agency (GPSA) and Shall be approved by the Tender Board or Delegated Tender Board"** Mwisho wa kunukuu

Orodha ya Wazabuni/maduka ni kama ifuatavyo-:

| Na | JINA LA DUKA | AINA YA BIASHARA | ENEO LILIPO | Na. YA LESENE YA BIASHARA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Bonifas Julius Mwendi | Uuzaji wa Vifaa vya Ujenzi | CHIKUYU | B 03376096 |
| 2 | Kikundi cha Karakana | Uuzaji wa Mbao | CHIKUYU | |
| 3 | Kikundi cha Gypsum | Watenegezaji na Wauzaji wa Mikanda ya Gypsum | MANYONI | |
| 4 | Peter Odiambo Boazi | Uuzaji wa Vifaa vya Ujenzi | BAHI | 03401006 |
| 5 | Tisa Hardware | Uuzaji wa Vifaa vya Ujenzi | KILIMATINDE | 3269317 |

Wajumbe baada ya kupitia walipisha maduka haya yatumiwe kama sheria inavyoelekeza kwani yatapunguza usumbufu unaojitokeza kwa baadhi ya mashule na zahanati kusafiri kwa umbali

mrefu kufata huduma ambayo wanaweza kuipata jirani na maeneo yao ya miradi pia walisisitiza bei zitakazo tumika ziwe za soko na dhamani halisi ya fedha ionekane .

**MUHT.NA. 29/2021/2022: KUJADILI NA KUPITISHA MANUNUZI YATAKAYO FANYIKA KWA UJUMLA (BULK PROCUREMENT) UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO UVIKO 19 KWA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI.**

Katibu aliwasilisha maombi ya ununuzi wa Vifaa Vya ujenzi kwa ajili ya Utekelezaji wa Mradi wa Mpango wa maendeleo ya Uvico 19 kwa shule za Msingi na sekondari Vifaa hivyo ni Mbao, Mabati na Tofali

A. Ununuzi wa Mbao wazabuni walioomba ni kama ifuatavyo:-

| Na. | JINA LA MZABUNI | KIASI |
|---|---|---|
| 01. | FIVE BROTHERS HARDWARE - Manyoni | 242,968,000.00 |
| 02. | G.J.SWAI WOOD WORKING & BUILDING MATERIALS SUPPLY-Manyoni | 253,374,000.00 |
| 03. | JUMANNE ALLY MALIWATA HARDWARE & GENERAL SUPPLY - Manyoni | 236,567,100.00 |
| 04. | KAPUGI GENERAL SUPPLIES - Mafinga | 210,685,200.00 |

Wajumbe baada ya kupitia waliridhia kazi hii ya mbao ifanywe kwa pamoja "Bulk Procurement" Kutoka kwa Mzabuni **Kapugi General Supplies – Mafinga** kwani gharama zinapungua kulinganisha na wazabuni wenyewe bei hii ni ya mpaka Kufikisha Mzigo Manyoni

B. Ununuzi wa Matofali

| Na. | JINA LA MZABUNI | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | FIVE BROTHERS HARDWARE | 1,500 @ |
| 2 | JAMES KIMOLO GENERAL SUPPLY | 1,500 @ |
| 3 | SIRILI BERNARD MALLYA | 1,700 @ |
| 4 | JESHI LA MAGEREZA MANYONI | 1,500 @ |

Wajumbe baada ya Kupitia na kujadili waliamua kuwa Wazabuni watatu waliolingana bei wote wafanye kazi ya kuuza tofali kwa shule za msingi, Sekondari na Hospitali ya Wilaya ili kurahisisha kazi kwani tofali zinazotakiwa ni nyingi. Kiasi cha tofali 157,300. Hivyo walimu waelezezwa kununua tofali kwa **FIVE BROTHERS HARDWARE, JAMES KIMOLO GENERAL SUPPLY** na **JESHI LA MAGEREZA MANYONI**

C. Ununuzi wa Bati

Katibu aliwasilisha taarifa ya Ununuzi wa Bati Kutoka Alaf Tanzania Ltd aina ya Simba Dumu kwani ndio bati yenye ubora unao kubalika ukilinganisha na aina nyingine za Mabati, Wajumbe waliafiki na Kupitisha kuwa Bati zinunuliwe Alaf kwa bei ya punguzo ya Tsh. 30,218 @ Badala ya Tsh.35,550.

**MUHT.NA. 30/2021/2022: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.**

Hakukuwa na Mengineyo

**MUHT. 31/2021/2022: KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 09:30 Alasiri kwa kuwashukuru Wajumbe wote wa Bodi ya Zabuni waliohudhuria na kusisitiza yote yaliyojadiliwa na Wajumbe yazingatiwe.

**U M E T H I B I T I S H W A**

..............................

Dennis L. Mmbando
KATIBU

TAREHE...11/11/2021

..............................

Ramlah Munisi
MWENYEKITI

TAREHE...11/11/2021